**Learning by Ear – Sikiliza na Ujifunze**
**04 – Cars and Bicyles ( Magari na Baiskeli )**
**Text: Richard Lough (anatamkwa Lock )**
**Redaktion und Idee: Johannes Beck**
**Translator: Mohamed Dahman**

---

Hujambo msikilizaji! Karibu katika mfululizo wa vipindi maalum vya Skiliza na Ujifumze kuhusu mazingira ambapo leo tutaweza kufahamu kwa nini gari ni mojawapo ya chanzo kikuu cha uchafuzi wa mazingira kutokana na utowaji wake wa gesi ya carbon dioxide. Tutafahamu kwamba carbon dioxide ni mojawapo ya gesi zinazoathiri mazingira ambazo wanasayansi wanasema zinasababisha dunia kupata ujoto mkubwa kwa mchakato unaojulikana kama kuongezeka kwa kiwango cha ujoto duniani. Kwa vile tuanalitegemea mno gari katika kutufikisha hapa na pale wakati wa safari zetu ni nini suluhisho? Tutaangalia faida za kutumia huduma za usafiri wa umma na hata baisikeli. Leo katika Radionovela pia tutaangalia usafiri wa anga na taathira mbaya kwa dunia kutokana na kuongezeka kwa kiwango cha ujoto duniani. Na mwishoni mwa kipindi hiki kilichotayarishwa na Richard Lough (anatamkwa Lock) tutajielimisha zaidi carbon dioxide ni kitu gain, kwa nini tunaihitaji, lakini wakati huo huo isiwe nyingi mno.

**Music – 0:30**

**Radionovela**

**SFX Road Traffic…….. Sauti ya Magari Barabarani**

**Moses:** Kuna siku nataka niendeshe gari la aina ya jeep!

**Monica:** (*teasing ….akitania*) Unasema nini Moses? Huachi wee… daima utaishia kutumia basi tu! Ama kwa mimi usinitazame kwa woga… nitaendesha gari aina ya Toyota Prado, mjigari mkubwa unaotamba barabarani!

**Moses:** Hapana, hapana, hapana! Monica unakosea hapo! Nimejipangia niwe mfanyabishara tajiri na nitajidai na utajiri wangu! Nitamiliki gari aina ya Hummer… hilo ni gari kubwa kabisa… kipimo cha utajiri… linalotamba barabarani leo hii.

**Gladys:** Nini…Moses… Hummer ndo gari gani hilo?

**Moses:** Hummer…Gladys ni gari la kijeshi la Kimarekani. Na hivi sasa ndio yamegeuzwa kuwa magari ya kawaida kutanua barabarani. Na umeipata hapo kwamba David Beckam mchezaji soka mashuhuri wa Uingereza anamiliki moja!

**Monica:** Ndiyo… na hivi sasa pia limekuwa gari linalopendwa na vigogo wa Afrika…

***(collective laugh …….kicheko cha pamoja )***

**Monica:** Sio vibaya… inafaa hasa unapokuwa tajiri ukamiliki gari la maana… Wenye kijicho tena hapo kazi kwao!

**Moses:** Na isitoshe barabara zetu hazitunzwi… mashimo ndio maskani yake… kwa hiyo unahitajia gari la four wheel kwa ajili tu ya kutanua nalo mjini!

**Gladys:** Lakini vipi mmefikiria juu ya suala la uchafuzi unaosababishwa na magari ya aina hiyo?

**SFX Passing Truck ……Gari Kubwa la Mizigo Likipita…**

**Gladys:** (*coughs ….kikohozi* ) Hebu angalia moshi mweusi unaotolewa na gari hilo kubwa la mizigo! Uuuhhhh… nahisi mpaka mapafu yangu yanawasha!

**Moses:** Lakini moshi huo unapotelea mbali kwa kuchukuliwa na upepo… Hausababishi matatizo yoyote yale.

**Monica:** (*stunned …akionekana kushtuka* ) Hivi Moses unatania! Hukupeleleza safu ya ukungu uliochanganyika na moshi

ambayo mara nyingine hutanda juu ya mji wakati wa kibaridi cha asubuhi. Unataka kuniambia hukuwahi kuihisi hewa hiyo iliochafuliwa ikisababisha macho yako yachonyote?

**Gladys:** Lakini hata hivyo baya zaidi ni uharibifu wa mazinigira unaosababishwa na moshi unaotolewa na magari. Huenda ukafikiri kwamba moshi huo hutoweka tu ndani ya hewa lakini hivyo sivyo inavyokuwa.

**Moses:** Mbona sikuelewi Gladys…

**Gladys:** Mojawapo ya gesi inayokutikana kwenye moshi wa magari ni carbon dioxide.

**Monica:** Hiyo ni mojawapo ya gesi zenye kuathiri mazingira ama sivyo Gladys?

**Gladys:** Ndio hasaaa… Monica!

**Moses:** Mnaziitaje?

**Gladys:** Tunaziita gesi zenye kuathiri mazingira… tafadhali Moses usitake kutuambia kwamba ati hukuwahi kusikia juu ya gesi hizo zenye kuleta madhara kwa mazingira…

**Moses:** (*embarassed …akionekana kutahayari* ) Kusema kweli sikuwahi…

**Monica:** Ni vigumu kuelewa… lakini hivi ndivyo inavyokuwa: Kuna kundi la gesi ambalo huunda tabaka zito juu ya angahewa. Gesi hizi hulizuia joto kupenya kwenye angahewa ya dunia…

**Gladys:** Bila ya gesi hizi dunia inakuwa haiwezi kukalika kwa sababu joto lote litakuwa limeponyoka.

**Monica:** Lakini wakati tabaka hili la gesi linapozidi kuwa zito au nene ina maana joto jingi zaidi huwa linanaswa.

**Gladys:** Na matokeo yake ni ongezeko la kiwango cha ujoto duniani.

**Moses:** Na je magari ndio yanapaswa kulaumiwa moja kwa moja kwa athari za gesi zinazoathiri mazingira?

**Monica:** Hapana hatuwezi kusema moja kwa moja ni magari pekee. Kuna sababu nyingi kwa nini tunashuhudia kuongezeka kwa hali ya ujoto duniani kote.

**Moses:** Mfano ni upi…

**Gladys:** Kama vile kuchoma misitu… kuchoma mafuta ya petroli…

**Monica:** (*sarcastically …….kwa dhihaka ,,,,kejeli* ) Kwa hiyo inabidi tufanye nini… tupande basi ?

**Gladys:** Sawa kabisa. Hapa mjini hakuna sababu kwa nini tusipande mabasi. Na bora zaidi unaweza hata kutembea kwa miguu…

**Moses:** (*incredulous …… kwa kutoamini alichokisikia* ) Kutembea kwa miguuuu?

**Monica:** Hapo angalau imani yako itakuwa safi… kwani utakuwa hutoi gesi yoyote ile inayoathiri mazingira.

**Moses:** Unataka kutuambia nini… hebu mwenyewe angalia moshi unaotolewa na mabasi yetu.

**Gladys:** Ni kweli engine hizo za zamani ni chafu na zina uchafuzi mkubwa kulinganishwa na engine za kisasa. Lakini basi linapokuwa limejaa hapo tena unakuwa huchangii sana uchafuzi kwa kuzingatia takwimu za kila abiria kuliko vile inavyokuwa mtu mmoja kuendesha gari.

**Gladys:** Unaweza pia kuendesha baiskeli Moses… hiyo pia ni njia safi ya usafiri isioathiri mazingira.

**Monica:** Lakini Gladys nadhani barabara zetu ni za hatari sana kwa mtu kuendesha baiskeli. Hata hivyo nakubali kwamba inakuwa ni haraka zaidi kutumia baiskeli kuliko kutembea kwa miguu.

**Moses:** Hebu sikilizeni mazungumzo haya ya kufanya mazoezi yananifanya nihisi kiu. Hebu tukajipatie kinywaji cha soda pale mkahawani kwani nina miadi ya kukutana hapo na kaka yangu Quentin.

**X –fade from SFX Traffic in SFX Café ……..changanya sauti ya magari barabarani na halafu ya watu mkahawani**

**Moses:** Habari gani Quentin… huyu anaitwa Monica…

**Monica:** Habari…

**Quentin:** Nzuri Monica…

**Moses:** Na huyu ni Gladys…

**Quentin:** Hujambo Gladys…

**Gladys:** Sijambo… habari gani…

**Moses:** Nilikuwa nikiwaambia wasichana hawa warembo kwamba wakati nitakapotajirika nitaendesha gari aina ya Hummer…

**Quentin:** (*to the girls quietly …..akiwaeleza wasichana taratibu* ) Huyu jamaa… yuko ndotoni…

***(giggles from Monica na Gladys …..kicheko kutoka kwa Monica na Gladys)***

**Quentin:** Ohh mdogo wangu ungeliweza kuwa unasafiri kwa ndege kama mimi.

**Moses:** Quentin daima anakuwa safarini hapa na pale.

**Gladys:** Lakini hata safari za ndege ni mbaya zaidi kwa mazingira.

**Quentin:** Naelewa… na nakubali kuwa ni kweli. Unaju a nilisoma mahala fulani kwamba vyombo vya anga hufanya asilimia mbili ya gesi chafu ya carbon dioxide inayotolewa duniani. Lakini sina chaguo… Niko kazini.

**Gladys:** Ndio… lakini tatizo ni kwamba kuna watu wengine mamilioni kama wewe ambao wanasema hawana chaguo jengine. Usafiri wa vyombo vya anga yumkini ukawa unafanya asilimia mbili ya gesi chafu ya carbon dioxide inayotolewa…

**Moses:** (*slams down his glass …..anamkatiza kwa kugonga gilasi yake mezani* ) Ambacho ni kima kiduchu sana!

**Gladys:** Lakini ni chanzo kinachokuwa kwa haraka sana katika utoaji wa gesi zenye kuathiri mazingira duniani na shughuli zake zinadhoofisha juhudi zetu za kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa katika fani nyingine.

**Quentin:** Gladys, sipingi kile unachosema. Lakini unajua teknolojia za kisasa zinatuwezesha kutengeneza ndege safi zenye ufanisi zaidi wa utumiaji wa mafuta.

**Monica:** Lakini kama vile alivyosema Gladys kumekuwepo na ongezeko kubwa la watu wanaosafiri kwa ndege. Katika kupunguza hali hii hamuwezi labda badala ya watu kusafiri kwenda kukutana na watu wengine wawe badala yake wanatumia simu au hata ukanda wa video…

**Quentin:** Aaah lakini hiyo haiwezi kuwa sawa…

**Moses:** Mnasema gesi hizi zenye kuathiri mazingira zinaongeza kiwango cha ujoto duniani?

**Monica:** Ndiyo… kuna ushahidi wa kisayansi kuthibitisha hayo.

**Moses:** Athari hiyo iko kwa kiasi gani?

**Monica:** Hadi sasa wanasema ni pungufu ya asilimia moja … kwa kweli ni asilimia 0.7.

**Quentin:** Kima hicho sio chochote.

**Moses:** Kiwango cha joto cha wastani katika mji huu ni nyuzi joto 30 za Selsiasi. Kwa hiyo nyuzi joto moja ikiongezeka inaleta tafauti gani?

**Monica:** Kima hicho ni kikubwa sana. Hivyo hukugunduwa jinsi mienendo ya hali ya hewa yetu inavyobadilika? Jaribuni kuzungumza na mkulima yoyote yule atakwambieni kwamba hivi sasa sio jambo linalowezekana tena kutabiri hali ya mvua. Kizazi kilichopiua kilikuwa kikijuwa kwa uhakika ni siku gani ya kuvuna.

**Gladys:** Monica yuko sahihi. Na baadhi ya wanasayansi wanahofu kwamba ikiwa kiwango cha ujoto duniani kitaongezeka kwa zaidi ya nyuzi joto mbili… hapo hatutoweza tena kurekebisha mchakato huo. Je kwa hiyo bado unataka kumiliki gari la aina ya Hummer wakati utakapotajirika?

**Moses:** (*defeated …akionekana kushindwa* ) Sasa… mnanifanya nijihisi kama vile nina hatia… kama vile uharibifu wa gesi zenye kuathiri mazingira ni kosa langu… mambo hayo!

***(Monica/Gladys laugh …wanaanguwa kicheko)***

**Monica:** Bila ya shaka sio kosa lako Moses. Lakini lazima tutambue kwamba sote tunaweza kuleta mabadiliko katika kukabiliana na hali hiyo.

**Gladys:** Na ukweli wa mambo ni kwamba kuna njia za usafiri ambazo zina manufaa zaidi kwa mazingira kuliko nyengine lakini gari lako la Hummer sio miongoni mwa njia hizo Moses!

**Monica:** Nani aliekuwa tayari kurudi nyumbani?

**All (Wote):** Soteeeee…

**Moses:** Bila ya shaka nyote mtabidi muutwange… mtembee kwa miguu!

***(collective laugh …….kicheko cha pamoja )***

**Music – 0:30**

**Je ulikuwa ukijuwa ?**

Je ulikuwa ukijua kwamba huko nyuma katika karne ya 17 carbon dioxide ilikuwa ni mojawapo ya gesi za kwanza kabisa kuelezewa kuwa ni kitu kilicho tafauti kutoka kwenye hewa? Carbon dioxide ina sifa fulani mbaya kwa kiasi kikubwa kutokana na kuwa imeenea sana kati ya gesi zenye kuathiri mazingira. Na kama vile ulivyoweza kusikia hivi punde tu kwamba wanasanyansi wamekubaliana kwamba ongezeko la gesi zenye kuathiri mazingira linaongeza kiwango cha ujoto duniani. Lakini carbon dioxide ni gesi inayotokea kiasili katika angahewa ya dunia.

Kwa kweli iwapo carbon dioxide na gesi nyingine zinazoathiri mazingira zingelikuwa hazipo, dunia kama vile tunavyoijuwa ingelikuwa haikaliki. Wanyama wote, mimea, ukungu na viumbe hai viduchu kabisa huzalisha carbon dioxide wakati wa kupumuwa. Mimea baadae hutumia tena carbon dioxide kutengeneza sukari kwa kupitia utaratibu wa kutumia vitu vya mimea na viumbe hai fulani ambapo kwayo huunganishwa kutoka carbon dioxide na maji kwa kutumia mwanga wa jua. Kwa maneno mengine carbon dioxide ni sehemu muhimu katika mkondo wa carbon.

Tatizo linakuja wakati kunapokuwepo gesi nyingi mno za carbon dioxide katika angahewa.Kutokana  na harakati za binaadamu kama vile za kuchoma mafuta ya petroli, makaa na gesi ya asili vinavyotokana na viumbe hai vya wakati wa jiologia ya  kale, kuendesha magari,kurusha ndege na ukataji wa misitu,  mkusanyiko wa carbon dioxide hewani umeongezeka kwa takriban asilimia 35 katika kipindi cha miaka 200 iliopita kwa maneno mengine tokea enzi za kuanza kwa maendeleo ya viwanda. Baadhi ya wanasayansi wanasema huu ni mkondo tu wa

asili. Kwani kwa vyo vyote vile miaka milioni mia tano iliopita carbon dioxide ilikuwa imeenea mara ishirini zaidi kuliko ilivyo hivi sasa. Lakini watu wengi wanaitupilia mbali hoja hiyo na kusema kwamba mkusanyiko wa carbon dioxide hewani unaongezeka katika kiwango kisicho kifani.

Kudhibiti utoaji wa carbon dioxide duniani kote ni mojawapo ya changamoto kubwa zinazokikabili kizazi chetu. Lakini wanasiasa wanatafautiana juu ya njia bora za kufanikisha jambo hilo. Hata hivyo kile kinachoonekana kuwa ni cha uhakika ni kwamba iwapo tutashindwa kudhibiti gesi zenye kuathiri mazingira ongezeko la kiwango cha ujoto litaendelea duniani na hiyo kusababisha taathira mbaya sana kwa mazingira. Maeneo ya barafu ya ncha ya dunia yatayeyuka, viwango vya usawa wa bahari vitapanda na ukame utaongezeka vibaya sana.
Na je ni bara gani litakaloathiriwa zaidi? Naam wanasayansi wengi wanamini kwamba Afrika ndio itakayoathirika zaidi kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa licha ya kwamba mabara mengine ndio yanayohusika zaidi na uchafuzi wa mazingira duniani.

**Outro : Funga Kipindi**

Na hapo ndio tumekamilisha kipidi chetu maalum cha Sikiliza na Ujifunze kuhusu mazingira ambapo leo hii kimelenga magari na baiskeli. Kwa hiyo kumbuka kufikiria iwapo kweli kuna ulazima wa kutumia gari au basi tu linaweza kukidhi haja zako. Pengine unaweza hata kutembea kwa miguu au hata kutumia baiskeli. Iwapo utafanya hivyo utakuwa umetenda wema mkubwa kwa mazingira.Unaweza

kuleta mabadiliko na kuweka mfano kwa viongozi duniani wakati wakijadili namna ya kupambana na gesi zenye kuathiri mazingira.
Asante kwa kuwa nasi. Iwapo unataka kusikiliza tena kipindi hiki au kuwaeleza marafiki zako nenda kwenye tovuti yetu www.dw-world.de/be .
Kwaheri.